HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

MAWASILIANO.
Mkuu wa shule: 0735429246/0719429246
Makamu mkuu wa shule: 0746903246
Afisa Elimu Sekondari: 0758993762

SEKONDARI ZOGOWALE
S .L .P 30245,
KIBAHA.
07/04/2022

MZAZI WA
.....
.....

YAH: <u>FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI KIDATO CHA TANO 2022/2023</u>

Ninayo heshima kubwa kukufahamisha kuwa mwanao mtajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari kidato cha Tano 2022/2023 katika mchepuo wa …… katika shule ya Sekondari Zogowale iliyopo kata ya Misugusugu , Halmashauri ya Mji Kibaha, Mkoa wa Pwani. Ni matumaini yangu kuwa mwanao atakubali kuitumia vema nafasi aliyoipata. Shule itafunguliwa tarehe **……**. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni siku mbili kabla ya tarehe ya kufungua.

MAHALI ILIPO SHULE.
Shule ya Sekondari Zogowale ipo umbali wa Kilometa 7.5 kutoka Visiga Madafu ,kushoto kwa barabara kuu itokayo Dar se Salaam kwenda mikoani katika mtaa wa zogowale. Ukipanda basi toka mikoani shuka Visiga Madafu kisha vuka barabara upande wa kulia. Usafiri wa kukufikisha shuleni ni pikipiki ambazo zina gharama ya kati ya Tshs. 1,500/= na 2,000/=

Fomu zote zilizoambatanishwa na maelekezo haya zinatakiwa kujazwa kikamilifu. **TUNASISITIZA FOMU HII IREJESHWE BILA KUPUNGUZWA KURASA YOYOTE**. Fomu mbalimbali zimeambatanishwa ambazo zinahitaji kujazwa kwa ukamilifu. Wanafunzi wanatakiwa kufanyiwa uchunguzi hospital na fomu iliyoambatanishwa ya (medical examination) ijazwe kikamilifu na daktari. **TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE** pia zimeambatanishwa. Ni mategemeo yetu kuwa mwanao atazisoma kwa makini na kuzielewa.

A. MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

1. MICHANGO

i. Ada ya shule Tshs. 70,000/= kwa mwaka, 35,000/= kwa muhula
ii. Fedha za Tahadhali Tshs. 5,000/= haitarejeshwa.
iii. Mtihani wa Mock 20,000/-
iv. Fedha za Taaluma Tshs. 20,000/= kwa mwaka
v. Fedha za huduma ya kwanza Tshs. 10,000/= kwa mwaka.
vi. Malipo ya vibarua Tshs. 40,000/= kwa mwaka
vii. Fedha za Kitambulisho na picha Tshs.6,000/=
viii. Fedha ya nembo ya shule Tshs.2,000/=
ix. Ukarabati Tshs. 15,000/= hulipwa mara moja

Fedha zote ziwekwe katika account ya shule inayoitwa:-
ZOGOWALE SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT. Namba ya akaunti ni **21201200141** iliyoko katika benki ya NMB tawi la Kibaha Mailimoja. Fedha inaweza kuwekwa katika tawi lolote la NMB nchini. Wakilisha nakala ya karatasi ya benki shuleni mara baada ya kuweka fedha benki ili upatiwe stakabadhi. **KARATASI YA KUWEKEA FEDHA BENKI IANDIKWE JINA LA MWANAFUNZI TU MAHALI PA JINA LA MWEKAJI. NI MUHIMU ZINGATIA ILI KUEPUKA USUMBUFU.**

2. VIFAA VINGINE

Mzazi amnunulie mwanafunzi vifaa vifuatavyo.

i. Sketi mbili za kijivu mpauko **(LIGHT GREY)** ya kitambaa cha suti, ziwe zimeshonwa kwa heshima ndefu mpaka chini zisizoonyesha maungo, kwa ajili ya darasani zishonwe **V-SHAPE**. Sketi moja ya damu mzee, moja ya kijani kibichi hizi **ZISHONWE RINDA BOX** kwa ajili ya kazi za nje. Haya ndiyo yatakuwa mavazi yake kipindi chote atakachokuwa shuleni hataruhusiwa kuja na mavazi ya nyumbani.

ii. Scurf itakayoshonwa kwa kitambaa cha sketi ya kijivu. Ishonwe pembe nne.

iii. Shati 2 nyeupe mikono mirefu.

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye kisigino kifupi na sio mchuchumio. (flat shoes).

v. Soksi nyeupe zisizo na marembo

vi. Tshirts mbili zitapatikana shuleni

vii. Ndoo mbili kubwa na ufagio wa wima wa chelewa kwa wote

viii. Soft bloom na Squizer kwa wanafunzi wa mchepuo wa PCB na CBG

ix. Toilet brush na Hard bloom kwa wanafunzi wa mchepuo wa HGK

x. Soft bloom na reki kwa wanafunzi wa mchepuo wa HKL

xi. Ream mbili za karatasi aina ya A4 (PHOTOCOPY) kwa mwaka.

xii. Vifaa vya darasani

- Madaftari makubwa counter book 10 (3 quire).
- Wanafunzi watakaosoma mchepuo wa sayansi wanapaswa kuleta Dissecting kit, Mathematical set 1 na scientific calculator (1), kwa watakaosoma geography pia walete mathematical set na scientific calculator.
- Oxford advanced learners dictionary 1 kwa wanafunzi wa mchepuo wa Kiingereza na kamusi ya Kiswahili sanifu (1) kwa wanafunzi wa mchupuo wa Kiswahili.
- kalamu za wino za kutosha bluu au nyeusi na penseli.

xiii. Hijab kwa waislam rangi nyeupe kwa wenye kulihitaji vazi hilo.

xiv. Vifaa vya michezo Raba nyeupe na Jezi nyeupe zenye fito za blue, bukta na Tshirt.

xv. Pair za kitenge na sio kanga, pia taulo la kuogea.

xvi. Shuka nne, mbili za rangi ya light blue na mbili za rangi ya pinc pamoja na chandarua.

xvii. Track suit moja ya rangi ya kijivu na moja ya rangi ya pink zenye fito nyeupe pembeni kwa ajili ya masomo ya jioni(evening preparation) pamoja na soksi nzito za kujikinga na mbu.

xviii. Ndala za kuogea na masai sendals za muda wa ziada.

xix. Kila mwanafunzi anapashwa kuwa na sabuni za kutosha kwa ajili ya matumizi yake,sabuni za unga kwa ajili ya kufulia.

xx. Tochi na mwamvuli kwa ajili ya dharura,

xxi. Vyombo vya chakula - sahani, bakuli, kijiko na kikombe vyote vya aluminium(chuma).

xxii. Godoro futi tatu kwa sita na chandarua nyeupe pembe nne futi nne.

xxiii. RESULT SLIP

NB:

1. **VIFAA VYOTE VITAKAGULIWA WAKATI WA UTARATIBU WA KUMSAJILI MWANAFUNZI. TUNASISITIZA KUZINGATIA MAELEKEZO HAYA.**
2. **MWANAFUNZI ASIJE NA SIMU YA MKONONI HAZIRUHUSIWI SHULENI WALA HAKUNA SEHEMU YA KUZIHIFADHI MAWASILIANO NA WAZAZI YATAFANYIKA KWA KUTUMIA SIMU ZA SHULE.**

Nakutakia kila la kheri na maandalizi mema

MWAMBALLA T.A.
MKUU WA SHULE

HEADMISTRESS
ZOGOWALE SEC. SCHOOL
P. O. BOX 30245,
KIBAHA

3. SHERIA ZA SHULE

Katika jamii yoyote ile ni lazima kuwepo na **SHERIA , KANUNI na TARATIBU** zitakazowezesha jamii hiyo kuishi kwa kufuata maadili mema na mazuri ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

1. MAHUDHURIO.

i. Wanafunzi wote ni lazima wasome, waielewe na waifuate kwa makini ratiba ya kila siku.
ii. Kwa kuwa lengo ni kupata elimu , wanafunzi wote lazima wahudhurie na kuwahi vipindi vya darasani, vipindi vya elimu ya kujitegemea, michezo na shughuli nyingine zozote za shule kama zitakavyopangwa katika ratiba ya shule isipokuwa kama ruhusa ya kutokuwepo itatolewa.
iii. Iwapo mwanafunzi atakosa shule kwa sababu yoyote ile ni lazima siku inayofuata aje na taarifa ya maandishi kutoka kwa mzazi / mlezi au daktari kuelezea sababu za msingi zilimfanya asihudhurie shuleni siku hiyo/ hizo.
iv. Endapo mwanafunzi hatahudhuria shuleni kwa siku thelathini mfululizo bila taarifa yoyote atasimamishwa masomo na atafukuzwa shule kwa kutohudhuria siku tisini.
v. Pia mwanafunzi anaweza kufukuzwa shule kwa kukimbia/ kutohudhuria na kutofanya mitihani.
vi. Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya mazingira ya shule bila kibali maalum kitakachotolewa na mwalimu wa zamu/ darasa.
vii. Wanafunzi wote wanatakiwa kufuata ratiba ya sikuekwa usahihi, kuanzia saa 1:20 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri au kama itakavyoelekezwa vinginevyo.
viii. Wanafunzi wote wanatakiwa kushiriki shughuli zote baada ya ratiba ya darasani kama elimu ya kujitegemea, clubs, debates , michezo na usafi wa mazingira.

2. TABIA NA MWENENDO

Kuvunja miiko ifuatayo kunaweza kusababisha mwanafunzi kupata adhabu kali, kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa:-

i. Utoro
ii. Uzururaji
iii. Uasherati.
iv. Wizi na uongo
v. Kuvuta bangi au ulevi wa aina yoyote ile.
vi. Utumiaji madawa ya kulevya
vii. Kuchezea, kuharibu au kudharau alama za taifa kama bendera na wimbo wa taifa
viii. Kupigana au kutukana.
ix. Kutoa lugha ya matusi kwa yoyote yule
x. Kugomea masomo, adhabu na maagizo yoyote yanayotolewa na walimu.
xi. Fujo na uchochezi usio na msingi unaoweza kuharibu amani.
xii. Kutokufanya mitihani au mazoezi kwa makusudi na bila taarifa maalum
xiii. Kuficha maovu, waharifu na uhalifu.
xiv. Makosa ya jinai
xv. Kutoa mimba
xvi. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
xvii. Kuoa au kuolewa
xviii. Kutumia vibaya mali ya umma na hivyo kusababisha uharibifu na hasara.
xix. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mwl anayehusika na malezi ya wanafunzi.
xx. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi, Mawasiliano na wazazi yatafanywa kupitia makamu mkuu wa shule au na mwalimu mlezi atakayeelekezwa kwao. Mwanafunzi atakayegungulika kumiliki simu au vifaa vinavyoendana na simu kama line, battery au handset atachukuliwa hatua za kinidhamu.
xxi. Kukutwa/kukamatwa/kuhifadhi/kutumia simu ya mkononi kinyume na utaratibu wa shule.

3. HESHIMA.

i. Wanafunzi wote wanatakiwa kutii kengere.
ii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuvaa sare ya shule kwa unadhifu, kwa usahihi na kuchomekea wakati wote wanapokuwa katika sare ya shule. **ATAKAYEVAA AU SKETI FUPI ITAKATWA NA KUTEKETEZWA ILI KULINDA HESHIMA NA MAADILI YA TAIFA. Tunasisitiza heshima katika mavazi.**
iii. Wanafunzi wote wanatakiwa kusimama parade kwa unadhifu na ukakamavu.
iv. Wanafunzi wasimame kusalimia walimu au mgeni aingiapo darasani.
v. Wanafunzi wasitoke darasani bila ruhusa na kwa makundimakundi.
vi. Wanafunzi wasipige kelele darasani
vii. Wanafunzi waheshimiane wao kwa wao na wawaheshimu viongozi wao
viii. Hairuhusiwi kuzomeana darasani au nje ya darasa
ix. Wanafunzi wasalimiane na walimu au watu waliowazidi umri
x. Wanafunzi wawaheshimu wafanyakazi wengine waliopo shuleni pamoja na maeneo ya jirani yanayozunguuka shule
xi. Wanafunzi wawe mfano bora katika fani zote heshima, kazi na usafi hata wanapokuwa nje ya mazingira ya shule.

4. MAVAZI

i. Wanafunzi wote watavaa sketi za rangi ya kijivu mshono wa v- shape, shati nyeupe mikono mirefu pamoja na skaf za rangi ya kijivu wakati wa saa za darasani. Yatumike material ya kitambaa cha suti. Mwanafunzi ashone sketi mbili za darasani ndefu mpaka chini ili kujihifadhi. ANGALIA KIAMBATANISHO.
ii. Pia kutakuwa na mavazi maalum yatakayovaliwa baada ya saa za masomo na sio mavazi ya nyumbani. Wanafunzi wanapashwa kushona sketi moja ya rangi ya damu mzee na moja ya kijani kibichi(dark green). Mavazi haya yatavaliwa na T-shirts ambazo zitapatikana shuleni kwa rangi zinazoendana na sketi. Mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi.
iii. Kofia, viatu vya ghorofa na mapambo mengine haviruhusiwi.
iv. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi nadhifu. Wasichana hawaruhusiwi kusuka nywele.
v. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na kucha fupi za mikono na miguu. Rangi ya kucha hairuhusiwi.
vi. Mwanafunzi atakayekwenda kinyume na mavazi rasmi yaliyoidhinishwa atanyang'anywa na hatarejeshewa.
vii. Wanafunzi wote watavaa viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba na soksi nyeupe zisizo na marembo.
viii. Wanafunzi wote wanatakiwa kuleta kandambili kwa ajili ya kuogea tu na masai sendals za muda wa ziada.
ix. Haturuhusu marembo.
x. Hijab kwa waislam rangi nyeupe kwa wenye kulihitaji vazi hilo.
xi. Vifaa vya michezo Raba nyeupe na Jezi nyeupe zenye fito blue bukta na Tshirt.
xii. Pair za kitenge na sio kanga, pia taulo la kuogea.
xiii. Shuka nne, mbili za rangi ya light bluena mbili za rangi ya pinc pamoja na chandarua.
xiv. Track suit moja ya rangi ya kijivu na moja ya rangi ya pink kwa ajili ya masomo ya jioni(evening preparation) pamoja na soksi

5. UTUNZAJI MALI.

i. Wanafunzi watatumia vizuri mali na vyombo vya umma kama vitabu, madawati,meza viti na majengo kwa ujumla. Ni marufuku kuandika chochote katika mali hizo. Atakayekiuka na kujulikana adhabu kali itachukuliwa dhidi yake.
ii. Wanafunzi wana jukumu la kutunza mali yao wenyewe na ile waliyokabidhiwa kwa matumizi yao wawapo shuleni.
iii. Wanafunzi wote wanatakiwa kurejesha vifaa vyote vya shule kama vitabu na vinginevyo kila wakati shule inapofungwa kwa mapumziko.
iv. Ni marufuku kuhamisha kifaa chochote kinachoweza kuhamishika kutoka mahali pakepa matumizi yaliyoidhinishwa.Endapo vifaa vitahamishwa kwenye vyumba vya madarasa kwa ajili ya kujisomea virejehswe kwenye vyumba husika bila kuchanganywa kuepuka usumbufu.

NB. UPOTEVU AU UHARIBIFU WA KIFAA CHOCHOTE CHA SHULE UTALIPWA NA MHUSIKA KWA GHARAMA HALISI ZA KIFAA HICHO.

6. MIPAKA YA SHULE

i. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali. Wanafunzi watakaoishi bweni hawataruhusiwa kutoka nje ya maeneo ya shule mara watakapopokelewa shuleni mpaka shule itakapofungwa au kwa kibali maalum. Pia wanafunzi hawaruhusiwi kufika sehemu zifuatazo isipokuwa kwa ruhusa maalum:-

a. Chumba cha walimu
b. Ofisi zote za shule
c. Maabara
d. Jikoni
e. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

ii. Wanafunzi hawaruhusiwi kabisa kufika sehemu zifuatazo:-

a. Vilabu vyote vya pombe
b. Majumba ya starehe
c. Majumba ya kufikia wageni

iii. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoka nje ya maeneo ya shule yaliyozunguushia uzio bila kupata kibali. Atakayegundulika kutoka katika maeneo ya shule bila kibali atachukuliwa hatua.

7. CHAKULA.

Chakula cha wanafunzi kitapatikana shuleni. Hakutakuwa na chakula maalum. Wanafunzi wote watakula chakula kitakachopatikana shuleni.

8. MATIBABU

Wanafunzi walio katika utaratibu wa bima ya afya waje na vitambulisho vyao gharama za matibabu zitakuwa chini ya wazazi.

9. MABADILIKO YA MAJINA NA ANUANI

i. Endapo Jina na anuani ya mzazi/ mlezi vitabadilishwa kwa sababu yoyote taarifa itolewe shuleni ili rekodi za shule ziwe sahihi wakati wote na hasa wakati wa kupokea taarifa mbalimbali kwa wazazi/walezi kuhusu maendeleo ya wanafunzi.

ii. Majina ya wanafunzi yaliyopokelewa shuleni ndio yatakayotumika bila kubadilishwa.

iii. Jina la mwanafunzi linaweza kubadilishwa endapo tu shule itapokea hati maalum kuhusu kubadilisha jina. (hati ya mahakama).

KIAMBATISHO A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI.

1. Jina kamili la mwanafunzi kama lilivyotumika katika mtihani wa kidato cha nne .....
2. Tarehe ya kuzaliwa mwanafunzi. Tarehe..... mwezi ..... mwaka.....
3. Mahali alipozaliwa mwanafunzi.
   i. Kijiji.....
   ii. Wilaya.....
   iii. Mkoa.....

4. Kabila la mwanafunzi.....
5. Jinsia ya mwanafunzi.....
6. Dini yake.....
7. Jina la baba yake.....
   Nambari yake ya simu.....
8. Jina la mama yake.....
   Nambari yake ya simu.....
9. Kama analelewa na mlezi, Jina kamili.....
   Uhusiano na mwanafunzi.....
   Nambari yake ya simu.....
10. Shule ya sekondari alikotoka mwanafunzi.....
11. Jina la mwenyekiti wa serikali ya mtaa.....
    Nambari yake ya simu.....
12. Je ana magonjwa sugu? Kama ndio taja.....
    Anatibiwa hospitali gani.....

Jina la mzazi Sahihi

....

Tarehe.....

KIAMBATISHO B: WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

(ANUANI YA MZAZI)
.....
.....
.....

YAH: HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SHULE YA SEKONDARI ZOGOWALE.

Mimi .....(Jina la Mzazi /mlezi wa mwanafunzi), Mzazi/ mlezi wa.....(jina la mwanafunzi)
Aliyekuwa akisoma shule ya .....(taja jina la shule aliyosoma mwanafunzi) katika wilaya ya ..... mkoa wa..... Ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari Zogowale iliyoko katika mji wa Kibaha kwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli nyingine zote za shule akikaa shuleni kwa kipindi chote cha miaka miwili cha kidato cha tano na cha sita.
2. Kwamba kwa muda wote huo wa miaka miwili sitamsumbua Mkuu wa shule, Afisa Elimu Sekondari Wilaya na Mkoa kuomba uhamisho.

Sahihi ya mzazi **Tarehe**

..... **.....**

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi .....Nimekubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Zogowale. Ninaahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu SHERIA,KANUNI na TARATIBU halali zilizopo. Pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi wa shule na wanafunzi wenzangu katika kuendeleza taaluma na shughuli nyingine nitakazopangiwa

Jina la mwanafunzi Sahihi

....

Tarehe.....

NAKALA.

1. Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kibaha
   S. L. P 30112, kibaha.
2. Afisa Elimu Mkoa ,
   S. L. P 30080,
   Kibaha - Pwani.
3. Mkurugenzi,
   Elimu ya Sekondari
   Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa,
   Dodoma.
4. Mkurugenzi,
   Elimu ya Sekondari,
   Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi,
   S. L. P 9121,
   D'SALAAM.

KIAMBATISHO C: STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM

MINISTRY OF EDUCATION , SCIENCE AND TECHNOLOGY
KIBAHA TOWN COUNCIL
ZOGOWALE SECONDARY SCHOOL, P O BOX 30245, KIBAHA.

.

TO THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE

.....
.....
.....

Please, examine the under named student and note any medical complications towards her joining this school .

Student's name.....Age.....Class.....

.....
MWAMBALLA T.A.
THE HEADMISTRESS
ZOGOWALE SEC. SCHOOL

1. Blood (any infection noted) .....

   Blood group.....

2. Stool.....

3. Urine analysis.....

   (note pregnancy).....

4. Eyes (any eye defect).....

5. Ears (hearing strength).....

6. Chest.....

7. Abdomen.....

8. Heart disease.....

Any chronic complaints which needs attention of the school authority

.....
.....
.....

Name of the medical officer.....
Designation.....Signature.....

Station.....Date.....

Official stamp.....